TANGAZO LA SERIKALI NA. 445 la tarehe 6/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22(1)*)

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI MUNZEZE YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi Munzeze ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi Munzeze.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA BUHIGWE

MSITU WA HIFADHI MUNZEZE

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 140.25 au Kilometa za Mraba 1.40 Unakopatikana na Mipaka Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Munzeze linalopatikana Wilaya ya Buhigwe, Mkoa wa Kigoma kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2762 ya mwaka 2018 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikali Na. 445 (Linaendelea)*




Dodoma,
___24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*